## Barua wazi kwa munyampara wa mji wa Bukavu

Mwananchi Ndala wa Ndala, ulipofika hapa mjini Bukavu, tulikupigia kengele na kukupasha ya kuwa Bukavu siyo tu mjini wa kula nyama ya ngombe yenyi kukaangwa kwa mafuta kutoka Walikale na tomato ya Mudaka. Magumu ni mengi tuliongeza kusema.

Matatizo pamoja na maendeleo ya mji wa Bukavu ni mzigo unaochukua kwenyi kichwa chako. Tulijazwa na furaha wakati tuliposikia kuwa barabara toka Mosala mpaka Chimpunda ilianza kutengenezwa upya. Udongo walimwa kwa kiponda ama gari tunalozoea kuita majembe (bulldozer).

Wakaaji wa Kadutu kwa jumla na wale wa Funu kwa upekee wafurahi kuona kuwa huo mfereji wa Funu umeanza kutengenezwa nao. Wapo hakika kuwa nyumba zao hazitaendelea tena kubomoka. Hata hivyo, kuna bado walakini !

Ewe mnyampara wa mji wa Bukavu, kitu kinachotushangaza na kutuvunja moyo ni kuona bei ya vifaa vingi zaponda bila mipaka. Miongoni mwa vifaa hivyo twaweza kutaja mafuta ya petroli pamoja na mihogo. Bila kusahau nyama. Yule unayetoka kumkomboa alipima kupinga bei ya mihogo, lakini la !

Tuliposikia kwenyi redio kuwa unajitahidi kupinga wale tunaozoea kuita "Kaddafi" juu ya kupandishwa kwa bei ya mafuta ya petroli tulijazwa na furaha. Lakini, kitumaini na furaha yetu vilivunjika kisha siku chache. Kwa sasa wenyeji wa magari watutia lisani pembeni. Madereva wa ma taxi waanza kutulipisha sasa zaire 20 pahali pa 10. Wale wa ma Bus watuazimisha tulipe zaire 10 pahali pa sita hapo hawali. Wakaaji wa Bukavu wakuomba ufanye vyote uwezavyo kusudi ya kushusha bei ya taxi. Kwa kuweza jambo hilo, yafaa kwanza uchungue yale yanayofanyika kunako vituo vya kugawanya mafuta ya petroli mbele ya kupiganisha kwa vita vikali wale wachuuzi wa magendo wa mafuta ya petroli.

Ebu mwenyi kiti wa mji wa Bukavu, tumekwisha kutambua kuwa wachuuzi wa nyama nao hawapendi kuheshimu kanuni za serikali. Hapo majuzi tulisikia kwenyi mitambo ya Sauti/ ya Zaïre kuwa bei ya nyama imepangwa kwa zaire 70 kilo moja. Ulipochukua hatua ya kuvunja jambo hilo, wachuuzi wa nyama walianza kusaga meno. Wamoja kati yao wamechukua hata hatua ya kugoma kazi hiyo. Hata hivyo, hawapendi kuheshimu kanuni uliwatolea. Kwa ngambo yetu, tulitambua kuwa wapo wenyi kukuzarau. Twakungoja upate kumaliza vikwazo hivyo. Mifano ni mengi lakini hiyo miwili itakutolea mwanga kuhusu namna raia unaowaongoza wasongwa na kuangamizwa na wale wanaozoea kujiita "wenyi mali". Tumaini letu kubwa ni kuona unatuletea jawabu (solutions) juu ya matatizo yetu.

Alamsiki.

## Je umesikia...?

**KWAMBA kuna jamaa wanaopiga wengine juu ya kulipishwa madeni ? Jamaa mmoja ambaye aliombwa alipe deni ya rafiki yake mzungu, katika kilabu cha pombe "3 Z", alimvizia huyo mzungu na mpaka akamchonganisha. Kwa kujilipisha kisasi, ndugu huyo aliamua amuelezee rafiki yake "zaïrois" kuwa mzungu huyo alimteta na kumsemea maneno mabaya. Katika hasira na ulevi, jamaa M... alirukia mzungu na kumuonyesha kweli kile wangwana wazoea kuita "cha mtema kuni". Pua ya mzungu ilivimba sawa finyango ya bata na nyoka za tumboni mwake zikalia "mama nakufa". Ukiona huyo mzungu njiani utamsikilia huruma.**

**Kumbe kuna namna nyingi za kujilipisha kisasi Moja hiyo ya mwananchi B.B.**

# JUA

## Gazeti la Kivu

### Mnamo tarehe 20 mai 1985

### Chama cha mapinduzi "MPR" kimetimiza miaka 18

Ni kweli miaka 18 imetimu tangu hapo Marechali Mobutu kaunda kiserikali Chama cha mapinduzi "MPR" kunako jiji la N'sele mwaka wa 1967 tarehe 20 May baada ya kutangaza nia yake hiyo kwa wapasha - habari mjini Mbandaka jimboni Ekwatori. Kuundwa kwa chama hicho kimoja kinachowaunga wana - Zaïre katika jamaa moja. Hicho kitendo kilikuwa cha kupiga marufuku uwingi wa vyama (zaidi ya 44), kusaga vikali mchafuko uliokuwa nchini kutokana na ubaguzi wa makabila uliogawa nchi katika majimbo 21 na kumwaga damu ya wananchi, kupoteza amani, uhaki na kazi kwa raïa.

Nchini Zaïre kote sherehe za kumbukumbu zilianza siku ya posho tarehe 18 hadi 20 May 1985. Mjini Bukavu, siku ya posho kazi za usafi wa mji (Salongo) zilifanyika. Na siku ya Mungu, tarehe 19, michezo mbalimbali ziliendeshwa. Mashindano ya mbio ya wapakazi wa "pousse - pousse" chini ya uchunguzi wa mnyampara wa mji wa Bukavu na kuungwa mkono na shirika Bralima/Bukavu. Wa kwanza kati ya 70 alipewa kiasi cha zaïre 2.000, sanduku 10 ya vinywaji na wengine zawadi mbalimbali. Mashindano ya maringa na nyimbo za utamaduni na uhimizaji wa chama yalifanyika pia. Ni wahimizaji wa shirika ONPTZ ndi walijinyakulia ushindi wakifwata na hao wa Pharmakina, Bralima, SNCZ, INSS na FAZ. Mashindano hayo yote yalifanyika mbele ya mwananchi Edjonga, makamu wa liwali na liwali wa jimbo kwa muda, Mama Mwando na miongoni mwao wakuu mbalimbali wa jimbo. Tarehe 20 May, maandamano ya furaha yalifanyika. Wanachama toka mitaa ya Kadutu, Bagira na Ibanda walikutana kunako nafasi ya 24 Novemba. Hapo, liwali wa jimbo kwa muda aliwahotubia wanachama wa mji wa Bukavu. Katika hotuba yake, liwali Edjonga aliweza kutoa mafasirio muhimu juu ya kumbukumbu ya tarehe 20 May, hali ya nchi mbele ya tarehe 20 May 1967 manufaa ya kuundwa kwa chama cha mapinduzi "MPR" na kazi kilizoisha zifanya mpaka leo, mpaka kugeuka chama - serikali.

**Kivu ya Kaskazini**

Mjini Goma, wakaaji walisherehekea tarehe 20 May 1985 na Waziri mkuu Kengo wa Dondo, liwali Mwando na wakuu mbali mbali toka Kinshasa na penginepo.

Kwa nini Waziri mkuu kawa Goma ? Mwananchi Kengo wa Dondo aliwasili mjini Goma kwa kuzindua kiserikali kituo cha moto wa stimu toka Katana hadi Goma. Tuwakumbusha wasomaji wetu ya kuwa kazi za singa, minara na kituo cha hapo Katindo (Goma) ziliendeshwa na shirika Energoinvest ya Yugoslavia.

**Bisimwa L.B. Tserou**

## Michezo

### Kombe la Afrika la timu bingwa : Bilima Kaichakaza Cara

Siku ya Mungu tarehe 19 May 1985, baada ya kuisakanya Cara bao moja kwa sifuri (1 - 0) kwenyi uwanja wa Mapinduzi (Stade de la Révolution) kuko jamuhuri ya watu wa Kongo, Bilima ya Kinshasa (Zaïre) ilijinyakulia cheti cha kuendelea katika mapambano ya kugombea kombe la matimu bingwa barani Afrika katika mchezo wa marudio. Wasomaji wetu watakumbuka kuwa Bilima ilitoka sare (1 - 1) na timu hii la Aiglon Cara mjini Kinshasa tarehe 5 May 1985 katika pambano la kwanza.

Kulingana na daftari ya mapambano hayo, timu za Vital'O ya Bujumbura (Burundi) ilichakaza Sogara ya Gabon na kujipatia ushindi baada ya kuanguka mabawa (1 - 1) katika mchezo wa marudio. Na katika pambano la kwanza Vital'O lilisakanya Sogara (3 - 1). Na Zamalek ya Misri (Egypte) kalaza El Hilal ya Sudania mabawa (4 - 1) na (1 - 1).

**BISIMWA L.-B. Tserou.**

## Habari za popote

**Bukavu**

Kiongozi wa ofisi yenyi kuhusika na uchunguzi wa usafirishaji wa bidhaa mipakani (Ofida), aliwasili mjini Bukavu ambako aliongoza kazi za seminari juu ya elimu na maelezo kazaa kwa wafanyakazi wa ofisi hiyo. Kisha seminari hiyo, vyeti vilitolewa kwa washuriaji. Pia mashua moja aina "vedette" ilitolewa kiserikali na kiongozi huyo ili kazi za uchunguzi kunako ziwa Kivu ziendeshwe barabara.

**Ulaya**

Baba Mtakatifu wa Roma, Yohana Paulo wa pili katembelea nchi za Ubelgiji, Uholandia na Luxembourg (Benelux). Huko alipinga ukosefu wa haki, kazi na ubaguzi wa rangi. Hakusahau kuhubiri juu ya masikilizano na masaidiano kati ya watu.

**Bisimwa L.B. Tserou**

## Tuzungumuze

### Adabu kwenyi kisima cha kuogelea

Siku za leo huona huku na kule kufanyika visima vya kuogelea. Kuogelea, kweli, ni moja kati ya michezo kamili (sport complet) na inafaa kucheza kwani una mafaa mengi kwa afya. Kuogelea inamfaidia mtu yoyote: mzee ama kijana, mme au mke, mtoto na mkubwa wote waweza kuogelea na kuchota afya katika sporti hiyo.

Lakini kuogelea visimani si kama kuogelea mutonini. Kanuni ziko za kufwata. Ya kwanza jua kama kisima ni kwa wote na kwamba huogelea watu wengi kwa wakati ule moja. Kumbe shurti la kwanza : uwe mwenyi kuvikwa. Usivae, lakini, haizuru vazi gani. Usijitumbukizie ndani na kapitula au kifunga-maziwa ile yako ya desturi. Hapana ! Haipendezi. Vaa mavazi ya sporti hiyo (maillots de bain, bikini, etc...). Kabla ya kuruka majini jimwangilie maji katika vyumba ama mahali palipoainishwa kwa jambo hilo (douche). Usitumie sabuni wala kitambaa cha usafi unapooga kisimani. Usiteme majini, usitosheamo makamasi na hasa usikojoe ndani. Ukimaliza pangusa na kausha maji na umende katika vyumba vya kujivikia. Munapooga waume na wake si vema kujitoa kwa michezo isiyo halali.

**Kimengele Kimode.**